Ufemerali katika Nyimbo za Muziki wa Bongofleva nchini Tanzania: Mifano kutoka Nyimbo Teule

Steven Yesaya
Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mkuu Mihayo cha Tabora (SAUT-Tabora)

Ikisiri

Makala haya yamechunguza *ufemerali* katika nyimbo za muziki wa *Bongofleva* nchini Tanzania, mifano kutoka katika nyimbo teule za wasanii wa muziki huu ambao nyimbo zao zimeonekana kuwa na *ufemerali*. Istilahi *ufemerali* iliyotumika katika makala haya imetoholewa kutoka lugha ya Kiingereza katika neno "*Ephemeral*" likimaanisha hali ya kitu kupendwa sana, kuvuma na baada ya muda mfupi kitu hicho kuchuja na kupoteza mvuto au umaarufu wake. Nyimbo za muziki wa *Bongofleva* zinazotolewa na wasanii zina sifa ya *ufemerali* yaani pindi zinapotolewa hupedwa sana, huvuma na baada ya muda mfupi hupoteza mvuto na umaarufu wake kwa wasikilizaji. Data zilizotumika katika makala haya zilipatikana kwa kutumia njia kuu mbili yaani usaili na ushuhudiaji. Katika makala haya imebainishwa kuwa sifa ya *ufemerali* katika nyimbo za muziki wa *Bongofleva*, ni kitendo cha kuvuma na kuchuja baada ya muda mfupi. Hivyo makala haya yameonesha kuwa katika nyimbo za muziki wa *Bongofleva* imeonekana kuwa dhana ya mawanda mapana ya kupendwa na kuvuma inajitokeza zaidi katika nyimbo za muziki huu ikilinganishwa na aina nyingine ya nyimbo zinazoonekana kuendelea kupendwa licha ya kutungwa na kuimbwa miongo kadhaa iliyopita, mfano nyimbo za muziki wa dansi, maarufu kwa jina la *zilipendwa*.

Maneno Muhimu: Ufemerali, Nyimbo, Muziki, Bongofleva

Utangulizi

Kietimolojia neno *Bongofleva* ni neno lililotokana na muambatano wa maneno mawili kutoka katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza (Bongo+Flavour). Katika lugha ya Kiswahili neno "Bongo" likiwa limetokana na neno la msimu lenye maana ya Dar es Salaam (Tanzania) na neno Fleva limetoholewa kutoka katika katika lugha ya Kiingereza neno *Flavour* likiwa na maana ya ladha. Hivyo, *Bongofleva* ni neno lilioambatanishwa katika lugha ya Kiswahili likiwa na maana ya ladha ya Kitanzania yaani muziki wenye ladha ya Kitanzania. Hivyo, nyimbo zote za muziki wa *Bongofleva* ni nyimbo za muziki wenye ladha ya kitanzania kutokana na sifa zake ambazo zinapatikana Tanzania pekee. Aidha, muziki huu umekuwa ukifanana kwa kiasi fulani na muziki unaoimbwa na wasanii kutoka

mataifa mengine kama Kenya, Uganda na Rwanda. Aidha nyimbo hizi kwenye mataifa hayo hazitambuliki kwa jina la *Bongofleva*; jina hili linajulikana kwa nyimbo zinazoimbwa na wasanii wa Kitanzania pekee. Nyimbo za muziki unaoimbwa na wasanii wa mataifa mengine mbali na Tanzania hufahamika kwa majina tofauti. Nchini Tanzania nyimbo za muziki huu zilianza kuimbwa na wasanii kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1980 na kuendelea kushika kasi zaidi miaka ya 2000 ambapo ndipo yalipoonekana mapinduzi ya muziki huu. Historia ya ujio wa nyimbo za muziki huu inaonesha kukabiliana na vikwazo vingi kutokana na aina ya muziki huu kuhusishwa na suala la uhuni na uharibifu wa maadili ya Kitanzania. Kadri siku zinavyozidi kwenda mbele maendeleo ya muziki huu yamekuwa mazuri na kuwa kivutio kikubwa kwa watu wa rika zote kuanzia watoto, vijana na wazee. Nyimbo za muziki huu hivi sasa zimekuwa zikitumika kama sehemu ya burudani pamoja na shughuli za kijamii.

Mwanzoni kabisa kabla ya utambulisho wa jina la muziki huu uliweza kujipatia majina mengi, kuna baadhi ya watu waliuita *Hip hop* au *rap* ya Kitanzania, muziki wa kizazi kipya nakadhalika. Kutokana na majina hayo yaliyokuwa yakiutambulisha muziki huu, jina la *Bongofleva* na jina la muziki wa kizazi kipya ndiyo yaliyoweza kupenya zaidi na kushika mizizi hadi leo hii na kuzidi kuutambulisha muziki huu. Nyimbo za muziki wa *Bongofleva* ni nyimbo zenye kutumia lugha ya vijana ambao wanajulikana kama kizazi kipya na wenye kutumia lugha ya vijana katika nyimbo za muziki huu. Lugha ya vijana, kwa mujibu wa King'ei (2010), ni lugha ambayo hutumiwa na vijana wanapokuwa peke yao katika mazungumzo. Vijana wanapokuwa katika mazungumzo yao, hubuni matumizi mapya ya maneno na sentensi ambazo huzitumia katika nyimbo zao za muziki wa *Bongofleva*. Jina la muziki wa kizazi kipya ikiwa na maana kwamba, muziki unaopendwa sana na vijana ambao hasa huonekana kuwa ndio kizazi kipya cha leo (Omari 2009, Samwel 2012). Kuna baadhi ya nyimbo za muziki wa *Bongofleva* huimbwa na wasanii ambao si vijana yaani watu wazima, hii inatokana na sifa ya muziki huu kupendwa na watu wa kila rika. Hata hivyo, nyimbo za muziki huu nyingi zimekuwa zikivuma sana na kupendwa pindi zinapotolewa ijapokuwa umaarufu wake huwa wa mpito. Kupendwa, kuvuma na kuchuja kwa nyimbo za muziki huu ni sababu ya awali kabisa iliyochagiza makala haya ili kuonyesha kiini cha *ufemerali* katika nyimbo za muziki huu. Makala haya yatajikita kuangalia *ufemerali* yaani mambo yanayofanya nyimbo zipendwe, kuvuma na kujipatia umaarufu kisha kuchuja na kupoteza umaarufu na mvuto wake.

Sababu za Kuvuma kwa nyimbo za Muziki wa *Bongofleva*

Kimsingi hivi sasa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* zimejipatia umaarufu mkubwa sana ndani na nje ya Tanzania kutokana na matumizi ya nyimbo hizi katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Umaarufu wa nyimbo za muziki huu

umechagizwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, huku maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) hasusani televisheni, video, radio, simu na intaneti vimesaidia kusambaza na kuvumisha nyimbo za muziki huu. Nyimbo za muziki huu hivi sasa ni nyingi na zimeenea kwa kasi kutokana na wingi wa vyombo vya habari na urahisishwaji wa teknololojia ya kurekodi nyimbo za muziki. Kuwepo kwa studio nyingi ambazo zinauwezo wa kurekodi kwa urahisi nyimbo za wasanii ni moja ya sababu ya muziki huu kupata umaarufu wake kutokana na upatikanaji wake kwa urahisi. Uchunguzi wa awali kwa njia ya ushuhudiaji katika makala haya unaonyesha kuwa nchini Tanzania karibu kila wilaya nchini kuna studio bubu na studio rasmi ambazo zinatutumika kurekodi muziki kitendo kinachofanya nyimbo nyingi kutolewa kwa wakati mfupi.

Hali hii imeonekana kuwa tofauti na hali ya kurekodi muziki kabla ya kuibuka muziki huu ambapo teknolojia ya kurekodi ilikuwa chini huku kukiwa na uhaba wa studio. Uwepo wa studio bubu katika maeneo mengi nchini ambazo zinafanikiwa kurekodi nyimbo za wasanii wa muziki huu kwa kiwango kizuri na kurushwa hewani kupitia vituo vya radio za kijamii vilivyosambaa nchini kote bila kupitishwa na vyombo vya uhakiki wa kazi za Sanaa vimefanya kila wimbo unaotolewa na msanii kuwafikia wengu na kuendelea kujipatia umaarufu wake. Kiuhalisia, kila wimbo unapotungwa na kuimbwa na msanii kupelekwa katika baraza la sanaa ili kuhakikiwa kabla ya kuusambaza. Kutokana na wasanii kukiuka kanuni hiyo nyimbo wanazozitunga na kuziimba wanazisambaza kitendo kinachofanya baadhi ya nyimbo kupigwa marufuku huku ilhali nyimbo hizo tayari zimerushwa hewani. Malengo ya kamati ya uhariri katika Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ilikuwa ni kuzihariri nyimbo zote za wasanii kabla ya kurekodiwa, nyimbo zilizopaswa kurekodiwa ni zile ambazo zinafuata maadili ya kitanzania. Hali hii imekuwa tofauti katika nyimbo za muziki huu ambapo wasanii huzitunga na kuzirekodi na baadaye kuzisambaza bila kupata ithibati toka baraza husika. Umaarufu wa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* unatokana na mambo yafuatayo:

Upigwaji Wake

Makala haya yamebaini kuhusu umarufu wa muziki huu kuwa kitendo cha kupigwa mara kwa mara nyimbo za muziki wa *Bongofleva*, ni moja sababu inayofanya nyimbo za muziki huu kujipatia umaarufu kutokana na kuifikia hadhira kubwa kwa wakati mmoja. Nyimbo za muziki huu zinapotolewa na wasanii wake hupendwa na wengi kutokana na kupigwa mara kwa mara katika sehemu mbalimbali kama vile vyombo vya habari, majumbani, sehemu za biashara, vyombo vya usafiri. Upigwaji wa mara kwa mara kwa wimbo wa muziki huu, uchunguzi wa makala haya umebaini kuwa, wasikilizaji wa muziki huu wamekuwa na mazoea ya kupenda wimbo/nyimbo mpya pindi zinapotolewa na wasanii wake.

Watu wengi wamekuwa na mazoea ya kupendelea zaidi nyimbo mpya na kuzipiga mara kwa mara hali inayosababisha wimbo husika kuvuma na kujipatia umaarufu. Hali ya kupenda upya hasa katika nyimbo zinazotolewa na wasanii hawa, uchunguzi umebaini kuwa si jambo geni kwa wasikilizaji wa muziki huu. Halikadhalika, hali ya kupenda upya na kuvumisha vitu vipya kwa Watanzania si katika nyimbo tu, bali hata katika vitu na mambo mengine kama misemo, mavazi, vifaa mbalimbali kama simu ambapo pindi vinapotoka au kutolewa hupendwa na kutumika zaidi. Hivyo, kwa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* zinapotolewa, hupendwa na kupigwa mara kwa mara kitendo kinachofanya nyimbo za muziki huu kuendelea kuvuma na kujipatia umaarufu mkubwa.

Imebainika kuwa nchini Tanzania, baada ya kupitishwa kwa sheria ya kuhodhi matangazo ya redio na televisheni yaliyokuwa yakihodhiwa na serikali kupitia Radio na Televisheni ya taifa, na kuruhusu vyombo vya habari kumilikiwa na watu ama taasisi binafsi vimekuwa vikiupiga muziki huu na kuufanya uvume kila sehemu ya nchi na hata nje ya Tanzania. Mapinduzi ya ujio wa muziki huu zaidi miaka ya 1990 yalipata upinzani mkubwa kutopigwa kwenye vituo vya Radio ambavyo vilikuwa vikimilikiwa na serikali. Baada ya kuruhusiwa kwa vituo binafsi nchini Tanzania, mapokeo yake yamekuwa makubwa kutokana na vituo hivi kuupiga muziki huu mara kwa mara na kujipatia hadhira kubwa na kuufanya uvume. Maelezo hayo kuhusu upigwaji wa muziki huu yaliungwa mkono na mtoa taarifa alisema kuwa:

> …asili ya muziki wa *Bongofleva* ni kurap kwa Kiswahili, muziki huu una mchanganyiko wa vionjo vya Kimagharibi pamoja na Kiafrika ambao umekuwa na mvuto kwa watu wengi na kuufanya kuupenda na kuufuatilia kila hatua jinsi unavyoimbwa... hali ya upigwaji wake katika vyombo vya habari na maeneo tofauti kwa pamoja ndivyo vinavyosababisha kuulazima umma kuendelea kufuatilia na kupenda nyimbo za muziki huu. Siku hizi karibu kila mtu anausikiliza muziki huu kwa namna moja ama nyingine kitendo kinachoulazimisha muziki huu uendelee kuvuma (Mahojiano na Seleman Msindi au kama anavyojulikana kwa jina la Afande Sele).

Kupigwa mara kwa mara kwa nyimbo za muziki huu kwa vyombo vya habari kama radio na sehemu tofauti tofauti kama vyombo vya usafiri, majumbani, kumbi za sherehe na burudani vimechangia nyimbo za muziki huu, kijipatia umaarufu na kuvuma, kutokana na kuwafikia watu wengi. Hali ya upigwaji wa mara kwa mara kwa wimbo wa msanii unapotolewa katika vyombo vya habari au sehemu mbalimbali za kijamii zinafanya nyimbo zinapopigwa mara kwa mara kuendelea kujipatia umaarufu. Mfano wimbo uitwao *Muziki* ambao umeimbwa na msanii aitwaye Sharif Thabit a.k.a Darasa, Makala haya umeubainisha kuvuma sana kutokana na kupigwa mara kwa mara sehemu mbalimbali. Ushahidi huu

uliweza kutolewa na mtoa taarifa mmoja kwa njia ya mahojiano ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Jijini Dar es Salaam, katika mahojiano alisema:

> …unapousikiliza wimbo wa msanii Darasa ni mzuri hakuna asieupenda, ukiangalia mpangilio wa maneno ya wimbo huu lazima utafurahia. Umeona sherehe gani ukipigwa huu wimbo watu wote wanakaa chini bila kusimama kucheza na kushangilia. Hii inaonyesha jinsi gansi msanii alivyotumia akili nyingi kuwateka watu wote waweze kuupenda wimbo huu. Hivyo, hali hii ya wimbo kuufanya upigwe mara kwa mara kila sehemu hutulazimisha tuendelee kuupenda (mahojiano na Omari, tarehe 13/07/2018).

Kutokana na ushahidi wa dondoo hapo juu, Makala haya yamebaini kuwa, ili wimbo wa msanii unapoendelea kuvuma unatokana na upigwaji na kuwafikia watu wengi na kuwalazimisha kuendelea kuzisikiliza wimbo huo na kuufanya uendelee kuvuma. Halikadhalika, sababu hii ilizidi kuungwa mkono na mtoa taarifa mkazi wa manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, alisema:

> …hivi vyombo vya habari, radio na televisheni, vina nguvu kubwa ya kuufanya wimbo wa msanii fulani upendwe na watu wengi. Hii inatokana na upigwaji wa mara kwa mara na kuufanyia ‘promo’ wimbo husika. Hali hii inatokana na sababu kadhaa wa kadha, ikiwemo matakwa ya wasikilizaji wake au mtazamo wa mtangazaji mwenyewe juu ya wimbo wa msanii husika. Pia, wakati mwingine, japo kuthibitisha inaweza ikawa inahitaji utulivu zaidi, kuna tuhuma dhidi ya baadhi ya wasanii wenye uwezo kiuchumi kutumia pesa zao kugharamia kwa kulazimisha nyimbo zao zipigwe Radioni, kumbi za starehe na kufanya nyimbo zao kuvuma kwa kuilazimisha hadhira kuzisikiliza nyimbo hizo muda mwingi na kufanywa zipendwe bila kukusidia (Rajab Lufuke, mahojiano mkazi wa Songea mkoani Ruvuma).

Kukua na kuenea kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, hasa matumizi ya kompyuta yaliyorahisisha upashaji wa habari, yamefanya muziki wa *Bongofleva* kuvuma, kupendwa na kujipatia umaarufu kwa watu wengi ambapo mara nyingi watu hulazimika kuzisikiliza nyimbo za muziki huu bila ridhaa yao kutokana na kupigwa kila mahali. Hali hii hufanya nyimbo za muziki huu kuwafikia wengi na kuufanya zivume na kuendelea kupenda. Halikadhalika, hoja hii iliendelea kuungwa mkono na Msindi (keshatatwa) alisema:

> Nyimbo za muziki wa *Bongofleva* watu hulazimishwa kuzipenda bila hata wao wenyewe kujua kutokana na upigwaji wake wa mara kwa mara katika vyombo vya habari kama radio au katika sehemu za starehe kama vile kumbi za disko, sehemu za starehe kama Bar, pamoja na sehemu nyingine nyingi ambazo zinatumia muziki kama sehemu ya kiburudisho. Kwa mfano, leo hii ukizunguka maeneo ya hapa Morogoro mjini au hata

> pembezoni, ukifungulia radio utasikia nyimbo za Bongofleva zikisikika au maeneo kadhaa utasikia nyimbo za muziki huu zikipigwa. Hali ya upigwaji mara kwa mara inafanya wimbo unaopata nafasi ya kupigwa mara kwa mara kulazimika kupendwa na kuufanya uvume (Mahojiano na Selemani Msindi).

Uhai wa wimbo wowote ule hutegemea upigwaji na usikilizaji wake kutoka kwa hadhira yake, ili wimbo husika uendelee kujipatia umaarufu na kuvuma. Maendeleo haya ya sayansi na teknolojia yaliyoenea nchini ni matokeo ya kuwepo kwa vyombo vya habari, kama radio, ambavyo vimerahisha nyimbo kusafiri maeneo mengi na kufanya nyimbo ziwafikie wengi. Makala haya yamebaini kuwa wasanii hutoa nyimbo mpya kila siku na pindi zinapotolewa huvpendwa na kuvuma sana. Hivyo, nyimbo mpya zinazotolewa na wasanii wa muziki huu hupewa kipaumbele katika upigwaji wake katika vyombo vya habari pamoja na maeneo mengine yanayotumia muziki huu kama sehemu ya shughuli husika mfano biashara, kumbi za starehe na sehemu za sherehe mbalimbali ambazo, kwa pamoja, hufanya nyimbo zivume na kujipatia umaarufu.

Maudhui

Makala haya yameweza kubaini maudhui yanayopatikana katika nyimbo za muziki huu kuwa ni sababu inayofanya nyimbo hizi kupendwa na kujipatia umaarufu wake. Nyimbo nyingi walizozitunga na kuziimba wasanii wa muziki wa *Bongofleva* maudhui yake yanaonekana kuwagusa na kuzungumzia zaidi mambo ambayo yanapendwa zaidi na watu wengi. Katika kubainisha mambo ambayo yanaimbwa na wasanii hawa katika nyimbo zao kuwa ni mambo ambayo yapo na yanaigusa jamii na wanajamii kwa ujumla. Wimbo wa *Bongofleva* ukitolewa huvuma, na kujipatia mashabiki wengi kutokana na kitendo cha wasanii kuitazama jamii na kuiimbia yale ambayo wanayataka kama vile masuala ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii (Mwangosi, 2018). Kutokana na wimbo wa muziki wa *Bongofleva* kugusa nyanja ambazo zinamhusu kila mwanadamu moja kwa moja, wasanii wanapotunga na kuziimba nyimbo zao hugusia masuala hayo. Hali hii huwafanya wasikilizaji kuvutiwa nazo na kuendelea kuzisikiliza kila wakati. Matokeo ya usikilizwaji wa nyimbo hizi muda mwingi huzifanya nyimbo hizo kuendelea kuvuma na kujipatia umaarufu.

Baadhi ya maudhui yanayopatikana katika nyimbo hizo ni mapenzi, starehe, siasa, uchumi nakadhalika. Kwa pamoja mambo hayo yamefanya nyimbo za muziki huu kupendwa na kuzifanya kujipatia umaarufu mkubwa. Hoja hii iliungwa mkono na mtoa taarifa, mwandaaji na mtangazaji wa vipindi vya muziki wa *Bongofleva* katika Radio, ambaye alieleza kuwa:

> Wasanii wanaoimba nyimbo zinazowagusa watu wengi (jamii) moja kwa moja, nyimbo hizo hupendwa sana na kujipatia umaarufu mkubwa, tofauti na nyimbo ambazo haziigusi jamii au watu moja kwa moja.

> Hivyo, nyimbo huvuma kutokana na '*impact*' kwa mtu au jamii kwa ujumla. Kwa mfano, nyimbo za wasanii kama Profesa Jay (*Chemsha Bongo*), Jay Mo (*Maisha ya Boading*), Mwana FA (*Alikufa kwa Ngoma*), Ferooz (*Starehe*), nakadhalika, hizi ni nyimbo ambazo moja kwa moja mashairi yake yanahusisha jamii. Mtu anapousikia wimbo huo kwa mara ya kwanza atalazimika ausikie tena kwa mara ya pili, mara ya tatu na zaidi. Hali kama hii ndiyo inayofanya wimbo huo upendwe na uvume kutokana na kila mtu kutaka kuusikiliza mara kwa mara kutokana na kumgusa au kuigusa jamii moja kwa moja. Mambo yanayozungumziwa katika nyimbo hizo yapo na ni uhalisia katika jamii na matokeo yake, wimbo huo lazima uvume (Mahojiano na Samwel Davis Kiama).

Nyimbo ambazo wasanii wanaziimba kwa kuzungumzia masuala yanayowahusu ama kuwagusa wasikilizaji wake, nyimbo hizo hupendwa na kuvuma zaidi. Mfano, Makala haya imeweza kubainisha maudhui yanayopatikana katika wimbo uitwao *Parapanda* wa wasanii Roma Mkatoliki na Stamina (Rostam) katika wimbo huo, wasanii hawa wamejaribu kuyaimba mambo halisi yaliyopo na yanayowagusa wanajamii pindi wimbo huo ulipotolewa. Kutokana na mashairi hayo kuwagusa wengi, hiyo ndiyo sababu ambayo imeufanya wimbo huu kupendwa na wengi kutokana na maudhui yake kuwagusa wengi. Wasanii wa wimbo huu, wamekuwa na ubunifu mkubwa katika kufikisha maudhui ya kusadikika kisiasa kutokana na kukithiri kwa vitendo vya uvunjifu wa amani nchini Tanzania kama vile utekaji na mauaji kwa wananchi ambayo yanasemekana kutekelezwa na watu wasiojulikana. Yafuatayo ni mashairi ya wimbo *Parapanda* ambao utafiti umebainisha kupendwa na kuvuma kwake kunatokana na maudhui yake kuigusa jamii nzima:

Korasi

Wanamiliki visenti,
Mambo yamebuma mipango haieleweki
Kuna manabii feki, ramani hakuna kila kitu hakieleweki
Parapanda italia parapanda
Parapanda italia parapanda

Kupendwa na umaarufu wa wimbo *Parapanda*, umebainisha kuwa wasanii wameweza kuimba masuala ambayo yapo na yameleta mjadala mkubwa katika jamii ya watanzania ambayo yameonekana kuwakera na kuwagusa wengi. Katika uimbaji wake wasanii wameweza kuiteka hadhira ya wasikilizaji kwa ubunifu wa ughanaji wa mashairi ya wimbo husika ambao umeonekana kuwavutia wengi. Mbali na suala la utekaji, kuna mambo mengine mengi ambayo wasanii hawa wameyagusia ambayo yanawagusa wengi ambayo ni masuala ya kisiasa, ufisadi na uwajibikaji.

Umaarufu wa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* hutokana na ubunifu wa wasanii wa kuweza kutunga na kuimba nyimbo zinazohusu masuala yanayogusa maisha ya watu wengi. Kikawaida wasanii wa muziki hawatungi nyimbo za muziki wao kutoka kwenye ombwe, hii ndiyo sababu inayofanya nyimbo hizi kupendwa kutokana na kugusa mambo yanayohusu maisha ya mwanadamu yoyote.

Makala haya yameongozwa na nadharia ya uhalisia katika kubaini mambo wayaimbayo wasanii katika nyimbo zao ni mambo halisia amabayo yapo na yanawagusa wanajamii wengi. Suala la nyimbo hizi kupendwa na kuvuma kwake kunatokana na wasanii wenyewe kuzitunga nyimbo zenye kugusia masuala ya kijamii kama utawala, majigambo binafsi, mila na desturi, elimu na mapenzi na ndoa. Kuvuma na kupendwa kwa vitu si jambo geni katika jamii ya watanzania kama ilivyobainishwa hapo juu, vitu vingi hutokea huvuma na kujipatia umaarufu mkubwa kama vile viongozi wa kisiasa, bidhaa kama mavazi, magari, wasanii wenyewe au hata mtu binafsi kama vile Babu wa Loliondo, Dokta Shika, Pierre Liquid nakadhalika.

Katika makala iliyoandikwa na Dkt. Levy katika gazeti la Mwananchi la tarehe 17 Machi 2018, yenye kichwa kiitwacho *Siyo sanaa tu… mpaka mapenzi kama Big G*, mwandishi ameweza kubainisha hali ya kuvuma na kujipatia umaarufu mkubwa kwa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* kama ilivyo katika masuala mengine, kama anavyonukuliwa akidai:

> Siyo muziki tu pia mapenzi ya sasa yanakinai upesi. Yaani watu hawadumu kwenye uhusiano kama zamani. Nyakati za sasa na mazingira yake yanahatarisha neno upendo. Kinachotokea ni kwamba wanaume wanatongoza kirahisi wasichana. Na wasichana wanakubali kirahisi sana. Sasa kwa nini mwisho wa mapenzi uwe mgumu? Lazima uwe rahisi tu. Ndani ya mwaka jana tu, Aslay alitoa nyimbo nyingi sana. Wasafi na bosi wao Diamond walitoa nyimbo nyingi sana ndani ya mwaka mmoja. Kama "Bigi Jii" vile. Nyimbo zilibamba ghafla na kutoweka ghafla. Muziki wa sasa unaisha utamu haraka kama ambavyo uhusiano wa sasa unaisha utamu haraka kwa wapendanao. Utandawazi umekuja na faida kubwa sambamba na ukubwa wa matatizo (Gazeti la Mwananchi, uk 20).

Dondoo hilo linabainisha sababu zinazofanya nyimbo za muziki wa *Bongofleva* kujipatia umaarufu na kuvuma kutokana na mapokeo ya haraka haraka ya nyimbo hizi, ambapo matokeo haya yamesababishwa na maendeleo ya utandawazi uliosababisha maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa wasanii kuweza kutunga na kurekodi nyimbo nyingi kwa kipindi kifupi.

Sababu za Kuchuja na Kufifia kwa Nyimbo za Muziki wa *Bongofleva*

Kabla ya kuanza kuelezea sababu za *ufemerali* katika nyimbo za muziki wa *Bongofleva* yatupasa kwanza kurejelea kiundani kidogo dhana za *ufemerali* na *Bongofleva* kama zitakavyotumika katika makala haya. Dhana ya *Bongofleva* itajadiliwa na kuelezwa zaidi kama ilivyotolewa na wataalam mbalimbali na dhana ya *ufemarali* itajadiliwa kwa mtazamo wa kiutohozi kutoka katika lugha ya Kiingereza. *Ufemerali* ni istilahi ambayo imetoholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza. Kwa mujibu wa *Oxford Standard Dictionary* (2000) inaelezwa kuwa, "*Ephemeral is lasting or used for only a short period of time",* ikiwa na maana ya kudumu au kutumika kwa muda mfupi (Hii ni kwa mujibu wa tafsiri yetu yawezekana isiwe rasmi sana). Halikadhalika, *Britanica World Language* (1959:426) inaeleza kuwa *"Ephemeral is anything lasting for a very short of time,"* ikiwa na maana ya kitu chochote kinachodumu kwa muda mfupi (Hii ni kwa mujibu wa tafsiri yetu yawezekana isiwe rasmi sana). Makala haya yamebaini kuwa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* zina sifa hii ya *ufemerali* pindi zinapotolewa na wasanii wake hapa nchini Tanzania.

Nyimbo hizi zimekuwa na sifa ya kupendwa na kuvuma sana pindi zinapotolewa na wasanii, kisha kupoteza mvuto na umaarufu wake baada ya muda mfupi. Makala haya yamebaini kuwa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* ni nyimbo za msimu kama ilivyobainika kutoka katika nyimbo zilizotolewa na wasanii kuchuja na kupoteza umaarufu wake haraka mithili ya jojo (bazooka). Mwanzoni unapoitafuna jojo inakuwa na utamu, lakini punde tu, utamu huisha. Hali kadhalika nyimbo za muziki wa *Bongofleva* zinapotolewa na wasanii huwavutia wengi na kupendwa zaidi, yaani wimbo unakuwa mzuri kuusikiliza kila muda. Utamu ukishaisha ile ladha ya jojo huisha kama ilivyo kwa nyimbo za *Bongofleva* baada ya muda mfupi huchuja na kupoteza umaarufu wake. Kwa upande wa jojo mtu anaweza kuendelea kuitafuna jojo hata kama utamu umekwisha ikiwa ni lengo la kuchangamsha meno huku ikiwa haina utamu wala mvuto wowote mdomoni, hali hii ndiyo inajitokeza kwa wasikilizaji wa nyimbo zilizochuja na kupoteza umaarufu wake.

Dhana ya nyimbo ni dhana muhimu katika fasihi, dhana hii imechunguzwa na kujadiliwa na wataalam wengi wa fasihi. Kuna aina nyingi za nyimbo ambazo zinapatikana duniani kote na muziki wa *Bongofleva* ni sehemu ya kipera cha fasihi simulizi ya Kiswahili. Hivyo, kuna aina mbalimbali za nyimbo katika jamii mbalimbali na hutofautiana kulingana na dhima zake pamoja na uimbwaji wake. Halikadhalika, nyimbo ni moja wapo kati ya kazi za sanaa. Wamitila (2003:188) anasema:

> Sanaa ni ufundi wa hali ya juu wa kuwasilisha mawazo aliyonayo mtu kwa njia inayoweza kumwathiri anayeyaona matokeo yake. Kuna aina nyingi za Sanaa kama uchoraji, ufumaji, udarizi, uchongaji, ufinyanzi na FASIHI. Nyenzo ya fasihi ni LUGHA.

Kutokana na maana hiyo ya sanaa, ni dhahiri kuwa, nyimbo za muziki wa *Bongofleva* ni kipengele mojawapo cha sanaa ambacho hutumia lugha. Pia nyimbo ni kazi ya fasihi ambayo ni zao la kazi ya sanaa itumiayo lugha. Nyimbo ni muunganiko wa sauti ambazo zinatolewa na mwimbaji au waimbaji. Wimbo waweza kuambatana au usiambatane na ala za muziki endapo utaghanwa tu na mwimbaji. Mahadhi ya nyimbo huwa ya kishairi ambayo huwa ya kijamii zaidi kama vile kisiasa, kiutamaduni, kidini au la. Mara zote wimbo waweza kuimbwa na na mtu mmoja, zaidi au kundi la watu ambalo hujumuisha sauti mbalimbali. *Bongofleva* ni aina ya mkusanyiko wa mitindo ya miziki ya kimataifa inayopigwa nchini Tanzania (Bongo) kwa ladha (fleva) za kitanzania (Nganyagwa 2005). Ni aina ya muziki pendwa ambao unaimbwa na kupendwa zaidi na vijana ambao ndio kizazi kipya, na hii ndiyo sababu iliyochangia kwa muziki huu wa *Bongofleva* wakati mwingine kuitwa muziki wa kizazi kipya (New generation). Aidha Nganyagwa (khj) anaendelea kusema kuwa;

> "Muziki wa kizazi kipya (hasa baada ya Reggae na *Hip Hop* kuwa zimeshajitoa katika mkusanyiko huo), unaohusu vijana kuanzia wapigaji na wapenzi wenyewe wa mtindo huo".

Aidha dhana ya muziki wa *Bongofleva* inaweza kufafanuliwa kuwa ni aina ya muziki wa kizazi kipya ambao umeibuka nchini Tanzania kutokana na kuingia kwa muziki wa Hip hop kutoka nchini Marekani ambao ulianzishwa na wamarekani weusi. Hata hivyo, muziki wa *Bongofleva* umekuwa ukipata tafsiri mbalimbali katika jamii ya watanzania; miongoni mwa wataalamu hao wametoa tafsiri mbalimbali kuhusiana na muziki huu wa *Bongofleva*. Tafsiri hizo za *Bongofleva*, baadhi ya wataalamu hao wanajaribu kuita muziki wa vijana, muziki wa kizazi kipya, muziki wa kileo, muziki wa kitanzania (Suriano 2006; 2007 na Omari 2009, Samwel 2012). Lakini kwa ujumla mziki huu wa *Bongofleva* umekuwa mstari wa mbele katika kuleta haki na usawa miongoni mwa binadamu kwa kujadili matatizo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni yanayoikabili jamii. Muziki wa *Bongofleva* ni muziki unaopendwa na vijana na ambao huutumia katika kuelezea hisia pamoja na matatizo yao. Maelezo haya yanafafanuliwa na Omari (2008:73) anaposema:

> …vijana wengi wa Kitanzania pia hutumia muziki huu kuelezea matatizo yao ya kila siku kama: ukosefu wa ajira na athari zake, dola na nguvu zake, umasikini na kadhalika.

Muziki wa *Bongofleva* umeshamiri kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania kuanzia miaka ya 1990 hadi sasa kwani hapo awali muziki huu wa *Bongofleva* umekuwa umesambaa zaidi maeneo ya mijini lakini kipindi cha sasa muziki huu umeenea pande zote za nchi ya Tanzania. Muziki huu wa *Bongofleva* umekuwa na sifa kadhaa ambazo zimeainishwa na wataalamu wengi kama vile Chachage (2002), Majembe (1998) na Omari (2008, 2009). Sifa ambazo zimejadiliwa na

wataalamu hao ni pamoja na matumizi ya lugha ya mchanganyiko yaani kuchanganya lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni au kienyeji, majigambo pamoja na kuchanganya tamaduni. Hivyo basi, nyimbo nyingi za muziki wa *Bongofleva* zimeathiriwa na *ufemerali* ambapo baada ya kupendwa, kuvuma na kujipatia umaarufu huchuja na kupoteza mvuto wake. Miongoni mwa sababu zinazofanya nyimbo hizo kuchuja ni pamoja na:

Kwenda kinyume na Maadili ya Jamii

Nyimbo za muziki wa *Bongofleva* zinachuja na kupoteza umaarufu kutokana na wasanii wake kwenda kinyume na maadili ya jamii yaani mila na desturi za Watanzania. Wasanii wa muziki wa *Bongofleva* wanaonekana kutoenenda sawa na maadili ya kitanzania katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za muziki huu. Hali hii imeonekana kujitokeza sana katika haiba na mienendo ya wasanii wa *Bongofleva*, hasa katika mitindo ya uimbaji na uchezaji pindi wawapo majukwaani. Jamii ya Watanzania, wakiwemo viongozi, kwa kulinda maadili, utamaduni na desturi za taifa, hujikuta kukemea na kusababisha baadhi ya kazi za wasanii hawa kupigwa marufuku kusikika kitendo kinachofanya wimbo husika kupoteza mvuto wake kwa kuchuja na kufifia. Hali hii inapojitokeza, kazi za wasanii zinakosa uthamani katika jamii na hivyo kupoteza umaarufu wake katika matumizi ya kila siku.

Hivi sasa, kutokana na utandawazi ulioenea kila kona ya dunia na kufanya dunia kuwa kijiji, wasanii wa muziki huu wanaonekana kupoteza uzalendo na mwelekeo wa misingi ya utanzania katika kulinda na kudumisha mil ana desturi. Baadhi ya wasanii wamekuwa wakiigaiga kila kitu kutoka kwa wasanii wa Marekani katika uimbaji wa nyimbo za muziki wao, kuanzia jinsi ya uvaaji, uchezaji na hata staili za maisha wanayoyaishi. Wasanii hawa wanasahau kuwa Tanzania na Marekani ni vitu viwili tofauti ambavyo huwezi kuvifananisha. Utamaduni wa Wamarekani ni tofauti kabisa na utamaduni wa Mtanzania. Ndio maana hata ukirudi nyuma ukiangalia historia ya Tanzania, utaona ni tofauti kabisa na historia ya Marekani. Kwa mfano, uhuru walio nao Wamarekani katika mambo yao, huwezi ukauleta uhuru huo kwa Watanzania; huo sio utamaduni wa kitanzania. Ukiangalia miziki ya ng'ambo hususani Marekani na Ulaya, wasanii wake kitendo cha uchezaji nusu uchi katika nyimbo zao ni suala la kawaida kwao, kuvaa nusu uchi na kutembea mitaani wao huona sawa. Ukichunguza utamaduni wa Watanzania haupo hivyo, ndipo wasanii wa muziki wa *Bongofleva* wakiwaona hao Wamaekani huwaiga katika uimbaji wa nyimbo zao kama vile kuvaa mavazi yanayoonesha nusu uchi. Kitendo kama hiki kinavyotokea katika nyimbo za muziki huu kinafanya jamii kuendelea kuwachukia wasanii pamoja na nyimbo zao. Hali hii inafanya nyimbo hizo kupoteza umaarufu na mvuto wake.

Kutunga nyimbo zinazokwenda kinyume na maadili ya jamii ama wanatenda mambo yanayokwenda kinyume na maadili ya Watanzania, hufanya nyimbo hizo

kutopendwa na kuchukiwa na watu wengi. Hivyo, wasanii wa nyimbo hizo, huchuja, hufifia na wakati mwingine kupotea kabisa kutokana na kukosa mashabiki. Kwakuwa uhai wa nyimbo za muziki huu upo kwa mashabiki wataozitumia nyimbo husika katika shughuli mbalimbali. Hivyo, wimbo ukikosa mashabiki huchuja, hufifia na hupotea kabisa. Ikumbukwe kuwa msanii ni kioo cha jamii, hivyo, msanii ni daraja la jamii, kwa kuonyesha mila na desturi zinazopaswa kufuatwa na wanajamii wote kupitia kazi zake za sanaa. Msanii anapokengeuka kwenda kinyume na mategemeo ya wanajamii katika kazi zake, kazi hizo hupigwa vita na wakati mwingine kufungiwa kujihusisha na sanaa.

Wasanii wa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* wanapotoa nyimbo mpya wanapo bahatika kufanya mahojiano na watangazaji wa Radio na Televisheni mara zote ukisikiliza maneno yanayokosa uhalisia. Wasanii wengi hushindwa hata kujieleza kwa kile alichokiimba mwenyewe kutokana na kuimba mambo yasiyokuwa na maadili. Hivyo, msanii anapoimba nyimbo zinazokwenda kinyume na maadili ya jamii nyimbo hizo hukosa mapokezi mazuri kwa jamii na kuzifanya kuchuja na kufifia.

Halikadhalika, unenguaji unaofanywa na wasanii katika nyimbo zao kwa kuonyesha dhahili matendo yasiyokubalika pamoja na uonyeshaji wa maumbile ya miili yao, hususn kwa mabinti husababisha jamii kukosa imani na mvuto kwa kazi zao wapenzi na mashabiki wao. Unenguaji ni muhimu katika sanaa ya muziki, wasanii huchezesha miili yao kwa kuviringisha baadhi ya sehemu za miili kama kichwa, mikono, miguu, tumbo, makalio na kiuno (Masonga, 2005; Omari, 2009 na Samwel, 2012). Katika unenguaji, hasa wasanii wa kike wananengua kwa kuchezesha viuno na makalio yao, kitendo kinachochochea hisia za ngono, hii inaonekana kuwa ni ukiukwaji wa maadili ya Kitanzania na Afrika kwa ujumla.

Katika nyimbo za muziki huu baadhi ya wasanii, hasa jinsi ya kike huitumia vibaya miili yao, sababu inayofanya watu kukosa hamu ya kuendelea kusikiliza na kutazama video za muziki huu. Kitendo hiki ndicho ambacho makala haya yanabainisha serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara yenye dhamana kusimamia wasanii na kazi zao huchukua hatua za kuwafungia wasanii pamoja na nyimbo zao kuendelea kutumika ama kupigwa kwa namna yoyote ile. Kuna mifano ya nyimbo na wasanii ambao wameweza kufungiwa wao na nyimbo zao ama baadhi ya nyimbo zao ambazo zinakwenda kinyume na maadili. Makala yameweza kubainisha wimbo wa msanii Snura Mushi uitwao *Chura* kutokana na namna ya uchezeshaji wa maungo yao na mavazi waliyovalia ya uchezeshaji wa maungo yao, serikali kupitia wizara iliyopewa jukumu la kuwasimamia wasanii na kazi zao ilichukua jukumu la kuupiga marufuku wimbo *Chura* kuendelea kusikika kutokana na kwenda kimyume na maadili ya Kitanzania.

Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya starehe ambayo hupigwa muziki huu, wasanii wanaonekana kututumia miili yao vibaya kwa kuvaa mavazi ya nusu uchi au wakati mwingine wakicheza huku wakionekana mithili ya watu wafanyao ngono jukwaani. Kitendo cha wasanii kufanya mambo hayo, baadhi ya watu kuwachukia wasanii pamoja na kazi zao. Hili pia limejibainisha kwa baadhi ya wasanii wanapokuwa wanatengeneza video zao ambazo zimekuwa zikipigwa na wengi kuendelea kuzitazama kama ambavyo makala haya yameweza kubainisha baadhi ya watu kupinga uonyeshaji wa nyimbo hizo katika sehemu za wazi kama vile vyombo vya usafiri na majumbani.

Lugha yenye Matusi

Wasanii wengi wa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* katika tungo zao wamekuwa wakitumia maneno yenye matusi kitendo kinachowakera watu wengi, hivyo kitendo hicho husababisha wengi kuzichukia nyimbo za wasanii hawa. Nyimbo ambazo wasanii wake wamekuwa wakiimba kwa kutumia lugha iliyosheheni matusi zimekuwa hazipewi kipaumbele kupigwa mara kwa mara katika vyombo vya habari kama Radio na Televisheni kutokana na uzingativu wa maadili. Kitendo cha kutopigwa nyimbo za muziki huu zinafanya kukosa hadhira na mwisho wake kuchuja na kufifia kabisa.

Utamaduni wa Kitanzania umejengeka katika hali ya kuheshimiana na kuelewana ikiwa ni pamoja matumizi sahihi ya lugha safi na fasaha. Kwakuwa nyimbo hutumia lugha, lugha ndiyo nyenzo kuu inayoufanya muziki uweze kusonga mbele na kuweza kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Baadhi ya wasanii wa muziki huu wamekuwa wakitumia maneno yenye matusi katika tungo zao ambayo hayaleti staha kwa jamii ya Watanzania. Watu wengi kutokana na wasanii kutumia maneno yasiyokuwa na heshima katika tungo zao, hulazimika kutozifuatilia nyimbo hizo na kuzifanya zififie na wakati mwingine kufa kabisa kutokana na kwenda kinyume na maadili ya Kitanzania.

Makala haya yameweza kudondoa matini ya wimbo wa msanii Ney Wamitego uitwao *Shika Adabu Yako*. Katika wimbo huo, msanii amezungumzia masuala ya kijamii, lakini katika uwasilishwaji wa mambo hayo ametumia lugha isio na staha ambayo si utamaduni wa Kitanzania kuweza kutamka maneno hayo hadharani. Kwa kawaida msanii hutunga nyimbo za muziki wa *Bongofleva* kutokana na yale aliyoyaona, aliyojifunza na yale aliyoyasikia katika jamii. Kwa mantiki hiyo, msanii anapokuwa anatunga na kuimba nyimbo za muziki huu kwa kutumia maneno ya matusi, anakuwa anakiuka utamaduni wa jamii husika. Kwa mfano, maneno ya wimbo *Shika Adabu Yako* yameonekana kwenda kinyume na maadili ya jamii ya Watanzania, kama msanii anavyosema katika sehemu ya wimbo huo:

> Haya naanza kuchana, kuhusu wasichana
> Hawa ndio mama zetu ila sometimes hawana maana

Wapo wanaofanya muziki na muziki hauwalipi
Dada zetu wa mjini siku hizi hawavai chupi
Najiuliza ni joto au fashion
Au biashara ndo wanafanya promotion?
Aliokanja nikanjue, niwachane hawa ma-boy
We ni moto uliyewashwa, usiyezimwa hata kwa fire
Bongo Movie imekufa wamebaki kuuza sura
Wote wanataka kuimba ka Shilole na Snura
Ray Kigosi kawa mkongo hadi leo anaishi kwao
Hela za kuuza movie zote ananunua mkorogo

Katika wimbo huu msanii ametumia maneno ambayo yanamfanya mtu akiusikiliza wimbo asitamani tena kuusikiliza kutokana na kutumia maneno ya utusi kama **Dada zetu wa mjini siku hizi hawavai chupi**, ambayo yanaonekana kwenda kinyume na maadili ya Kitanzania kwa kuwadhalilisha wanawake hadharani. Katika mahojiano na mtoa taarifa, mkazi wa Mbezi, jijini Dar es Salaam, kutokana na kusikika wimbo uitwao *Kibamia* kutoka kituo cha Radio cha *East Africa* cha Jijini Dar es Salaam, katika mahojiano alieleza kuwa:

> …nyimbo hizi zimekuwa fasheni wasanii wamekuwa wakiimba nyimbo zisizokuwa na maadili kabisa. Ukiangalia hata uchezaji na uvaaji wa mavazi kwenye video zake ni balaa tupu na huwezi kaa angalia ukiwa na watoto sebuleni; ni aibu tupu katika uchezaji na uvaaji wao…ikumbukwe kuwa mila na desturi za Watanzania zilikuwa zimejengwa katika mazingira ya usiri mkubwa ambapo ilikuwa vigumu kwa mtu yoyote, hasa msichana, kuonesha sehemu za mwili wake.Hizi mila na desturi ndizo zilirithishwa toka kizazi kimoja hadi kizazi kingine, sasa hawa vijana wanaharibu kabisa (Mahojiano na Hamis, 23 Agosti, 2017).

Kuchuja kwa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* kunatokana na wasanii wake kukiuka maadili ya jamii kwa kutumia lugha ya matusi, uvaaji wa mavazi yanayoacha miili wazi na uchezaji usiokuwa na staha kama kukumbatiana mithili ya watu wafanyao ngono. Hali hiyo inawafanya watu wengi kuuchukia muziki huu na kuacha kuzisikiliza nyimbo hizo, matokeo yake nyimbo hizo huchuja na kupoteza mashabiki kama ilivyo katika wimbo *Shika Adabu Yako* ambapo msanii ameimba wimbo wake kwa kutumia lugha isiyo na staha.

Ukosefu wa Elimu ya Muziki kwa Wasanii

Elimu ya muziki ni kipengele muhimu sana kwa wasanii wote, wasanii wengi wa muziki huu wameonekana kukosa elimu inayoweza kuwafanya wakatunga na kuimba nyimbo zitakazo pendwa na kudumu kwa muda murefu kama ilivyo kwa baadhi ya nyimbo za muziki wa dansi zilizoimbwa kabla ya mapinduzi ya muziki wa *Bongofleva* lakini zinaendelea kudumu hadi leo hii. Wasanii wengi wanaingia kwenye fani ya utunzi na uimbaji wa nyimbo za muziki huu bila kuwa na misingi

ya elimu kuhusiana na muziki kwa ujumla. Wasanii wa nyimbo za muziki wamejikuta wakijihusisha na muziki kwa kuiga ama kumwiga msanii fulani ambaye yupo kwenye sanaa hii bila yeye mwenyewe kuwa na stadi za muziki kwa ujumla. Kuhusu hili, Afande Sele (keshatajwa) alinukuriwa akisema:

> Mimi sikuwa na wazo la kuwa mwanamuziki, nilijikuta nimeingia rasmi katika sanaa hii kwa kuvutiwa uimbaji wa Mr. II (Sugu). Katika uimbaji wangu hadi kuitwa Afande Sele leo hii; Sugu ndiye aliyenipa jina hili kutokana na background ya maisha yangu ambayo siwezi kuyaeleza.

Kutokana na dondoo hapo juu kutoka kwa msanii wa nyimbo za muziki huu, makala haya yameonesha wazi kuwa, wasanii wengi wamejiingiza katika sanaa hii kutokana na kuvutiwa na wasanii wengine tangulizi ijapokuwa suala la kipaji nalo linazingatiwa. Lissah (2007) kama ilivyonukuliwa katika Samwel (2012) anabainisha kwamba wasanii wengi wa muziki wa *Bongofleva* wameacha shule na kujiingiza katika muziki huu. Hali hii ndiyo inayofanya wasanii kutunga na kuimba nyimbo zinazokosa uhai wa kudumu muda mrefu. Ukosefu wa elimu ya muziki kwa wasanii inaonekana kuwa ndicho chanzo kikuu cha nyimbo kutungwa na kuimbwa kisha kuchuja haraka kutokana na wasanii wake kukosa elimu ya muziki. Muziki wa *Bongofleva* hivi sasa ni sehemu ya ajira kama ilivyo kwa ajira zingine kwa ajili ya kujipatia kipato ili kujikimu kimaisha bila kujifunza mihimili ya kazi ya muziki wenyewe.

Wasanii wengi wa muziki huu wanafanya muziki huu kimazoea ijapokuwa ni wasanii wachache sana wanaofuata misingi ya utunzi na uimbaji wake; wasanii amabao hawana elimu juu ya muziki wamekuwa wakitunga nyimbo zinazokosa mvuto kwa wasikilizaji wake. Nyimbo waziimbazo haziendani kabisa na kile wakiimbacho. Kwa mfano, ukitazama video za wasanii wengi hazina uhusiano na wakiimbacho na kile wakioneshacho katika picha zao. Kutokana na changamoto ya kukosekana kwa elimu ya muziki inayowakabili wasanii wa muziki wa *Bongofleva*, hulazimika kutengeneza kazi zilizo katika kiwango cha chini kiubora ambazo hazidumu masikioni mwa msikilizaji. Matokeo ya hali hii, kazi husika za muziki huu kukosa mvuto kuifanya hadhira kuzichoka kuzisikiliza.

Mapendekezo

Mbali na suala la *ufemerali* katika nyimbo za *Bongofleva* nchini Tanzania, hatuna budi kugusia mambo ambayo wasanii wa nyimbo za muziki huu ambayo wanapaswa kuyazingatia ili nyimbo zao wazitungazo na kuziimba ziweze kupendwa na kudumu kwa muda mrefu. Wasanii wa nyimbo za muziki wa *Bongofleva* wanatakiwa kutunga na kuimba nyimbo ambazo zinazingatia maudhui na mazingira halisi ya kijamii kwa kutunga nyimbo ambazo zinaangalia hali iliyopo katika jamii ili kufanya maudhui yake yaweze kudumu na kuendana na wakati kama ilivyokuwa kwa wasanii wa nyimbo za dansi ambazo ambazo

zilitokana na mazingira halisi amabayo wanadamu wanayaishi na kuyazungukia kila siku.

Serikali kuwa na chombo imara na Madhubuti kisicheteleka chenye kusimamia sheria na kanuni ambazo kila msanii anapaswa kuzifuata na kuziheshimu na kutoa ithibati kwa kila msanii ambaye atahitaji kutoa wimbo ambao utakuwa umepitiwa na kuhaririwa inapobidi. Chombo hicho ndicho kitakacho ruhusu msanii wa *Bongofleva* kutoa wimbo wake ama la kwa sababu kitaweka udhibiti miongoni mwa utitili wa wasanii ambao wanatunga nyimbo kila siku. Siku hizi kila mtu anaamua kutunga wimbo na kuurekodi bila hata kughakikiwa kama unakiuka maadili ya kitanzania ama la ila mradi tu ametoa wimbo wake na kusababisha nyimbo kukosa mvuto na kupoteza umaarufu wake.

Umasikini wa kipato umeonekana kuwa ni chanzo kikubwa cha wasanii wengi kutunga nyimbo ambazo zinavuma na kupoteza umaarufu wake kwa muda mfupi. Kwa kuwa wasanii wengi wamekuwa wakitunga nyimbo ili kujipatia kipato cha haraka ili kukidhi haja za maisha yao bila kujali uhai wa tungo zao kwamba zitadumu kwa kipindi kifupi au la. Wasanii kurekodi nyimbo bila kuiangalia jamii hutunga na kuimba nyimbo zinazokiuka maadili ya kitanzania ambapo mwisho huishia kuvuma kwa muda mfupi na kisha kuchuja kwa muda mfupi.

Hitimisho

Makala haya yamejadili sababu za *ufemerali* katika nyimbo za muziki wa *Bongofleva* nchini Tanzania. Katika makala haya tumechunguza sababu za msingi zinazosababisha wasanii wa muziki huu kutunga nyimbo ambazo zinavuma na kupendwa sana lakini katika kipindi kifupi, nyimbo hizo huchuja na kupoteza umaarufu wake. Muziki wa *Bongofleva* umekuwa ukikua siku hadi siku nchini Tanzania ambao ni matokeo ya athari za muziki wa kimagharibi hasa Marekani kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na kuwepo kwa soko huria. Katika uchunguzi wa makala haya imebainika kuwa kuingia kwa utanzu wa fasihi hii ya muziki wa Bongofleva nchini Tanzania ilikumbana na upinzani mkubwa kutoka kwa watu mbalimbali, kwani muziki huu kwanza kwake ulihusishwa na uhuni. Kwa mantiki hii, hivi sasa utanzu huu umekuwa muhimu na umekuwa sehemu ya ajira kwa watu wengi. Wasanii wa muziki wa huu wanatakiwa kutambua umuhimu wao kwa yale wanayoyatunga na kuyaimba ili yaendelee kudumu na kuendeleza umuhimu wake kwa jamii nzima.

Marejeleo

Chachage, C. S. L. (2002). "Ndani ya Bongo: Utamaduni na Migogoro ya Utamaduni". Paper presented at the Tenth Conference on the Political Environment in Tanzania, 17th September 2012, Dar es Salaam.

King'ei, K. na Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*, Nairobi: Kenya Literature.

Mwangosi, G. (2018). Kuchunguza Dhamira na Fani Katika Nyimbo za Magosi za Wanyakyusa. Shahada ya uzamivu (PhD Kiswahili Thesis Haijachapishwa), Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Majembe, A. K. (1998). "Language Use in the Tanzanian Hip hop Scene". Unpublished Research Paper, University of Dar es Salaam.

Mwanjoka, G. (2011). Harakati za Bongo Fleva na Mapinduzi. Dodoma: H.M Bureau.

Neill, M. O. (2007). Ephemeral Art: Mourning and Loss. Doctoral Thesis, Loughborough University.

Omari, S. (2006). "Mtindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania", Kiswahili vol. 69. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research. Pg 73-92.

Omari, S. (2009). Tanzanian Hip Hop Poetry as Popular Literature. *PhD Thesis* (Literature) University of Dar es Salaam.

Oxford (2000). *Advanced Learner's Dictionary*. New York: Oxford University Press.

Perullo, A. (2003). "The Life that I Live: Popular Music, Urban Practices, and Agency in Dar es Salaam, Tanzania", *PhD Dissertation*, Indiana University.

Samwel, M. (2012). Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi na ya Bongo Fleva". (Haijachapishwa), Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Suriano, M. (2005). "Muziki wa Kizazi Kipya, Tanzanian Youth Culture and Globalization", *Paper presented at the 75 Years Jubilee Symposium* (Institute oa Kiswahili Research 75 Years), Dar es Salaam, 4th-7th July, 2005.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*: Nairobi: Focus Publications.